JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2022

# URAIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2022

# 612 URAIA

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ........ 2

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Dola ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Dola ........ 4
2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu ........ 7
2.1.4 Swali la 4: Utamaduni Wetu ........ 10
2.1.5 Swali la 5: Uchumi wa Tanzania ........ 13
2.1.6 Swali la 6: Uhusiano wa Kimataifa ........ 15
2.1.7 Swali la 7: Uhusiano wa Kimataifa ........ 18
2.1.8 Swali la 8: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia/Kujifunzia Somo la Uraia ........ 20
2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia ........ 23
2.1.10 Swali la 10: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 25
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma na Utaalamu) ........ 28
2.2.1 Swali la 11: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia ........ 29
2.2.2 Swali la 12: Utamaduni Wetu ........ 34
2.2.3 Swali la 13: Upimaji na Tathmini ........ 40
2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia ........ 46

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........ 51

4.0 HITIMISHO ........ 52

5.0 MAPENDEKEZO ........ 52

Kiambatisho A ........ 53

Kiambatisho B ........ 54

# DIBAJI

Taarifa hii inachambua majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la A Mwaka 2022 kwa somo la Uraia. Taarifa hii imeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania ili kuwawezesha wanachuo, wakufunzi, wakuu wa vyuo, wathibiti ubora, maafisa elimu, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kufahamu changamoto zinazowakumba watahiniwa katika kujibu maswali ya mtihani. Ufahamu huo utawawezesha kutafuta mbinu za kutatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mtihani huu ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kimsingi, majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu katika Daraja hili.

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika somo hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 99.81 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu. Ufaulu huu mzuri umechangiwa na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa, umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki na umakini katika kusoma na kuelewa matakwa ya swali. Pamoja na watahiniwa kufanya vizuri katika mtihani wa somo la Uraia, wapo wachache walioshindwa kujibu vizuri baadhi ya maswali. Sababu kubwa zilizowafanya watahiniwa kushindwa kujibu maswali hayo vizuri ni kukosa maarifa ya kutosha katika dhana zilizotahiniwa, kutoelewa vema matakwa ya swali husika na kushindwa kutoa hoja zenye mantiki.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.



Athumani S. Amasi
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani huu wa somo la Uraia kwa Watahiniwa wa Ualimu Cheti Daraja A ulifanyika mwezi Mei, 2022 na uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Uraia wa Mwaka 2009 na fomati ya mwaka 2022. Mtihani ulikuwa na maswali kumi na nne (14), ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika Sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) yenye jumla ya alama 40 na kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B ilikuwa na maswali manne (04) yenye jumla ya alama 60 na kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15).

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni 'vizuri', 'wastani' na 'hafifu'. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Takwimu zinaonesha kuwa somo hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa kati ya watahiniwa 4,644 waliofanya mtihani, watahiniwa 4,635 (99.81%) walifaulu kwa kupata wastani wa alama 40 na zaidi na watahiniwa 9 (0.19%) hawajafaulu. Ufaulu huu umepungua kwa asilimia 0.14 ikilinganishwa na ufaulu wa Mwaka 2021, ambapo asilimia 99.95 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa Uraia. Sampuli za majibu yao zimeambatishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, taarifa inaonesha pia sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia kwa mada hizo ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani yao.


## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu)

Katika sehemu hii, kila swali lilikuwa na jumla ya alama 4. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Aidha, mtahiniwa alifaulu kwa wastani endapo alipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 3 hadi 4.

#### 2.1.1 Swali la 1: Dola


Swali lilimtaka mtahiniwa kuainisha majukumu manne ya Mahakama Kuu ya Tanzania kwa wananchi. Jumla ya watahiniwa 4,669 (100%) walifanya swali hili. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 96.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 – 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, asilimia 3.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 22.0 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 74.1 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 3,458 sawa na asilimia 74.1 waliweza kuainisha majukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania kwa wananchi kwa hoja tatu hadi nne. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Dola, hususan kipengele cha Mahakama na walielewa vema matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu sahihi. Mfano wa majibu sahihi yaliyotolewa ni; *kusikiliza makosa ya jinai, kushughulikia kesi za kikatiba, kushugulikia rufaa kutoka mahakama za wilaya na mahakama za hakimu mkazi, kutafsiri sheria zinazotungwa na Bunge* na *kutoa amri ya kufidiwa kwa watu walioathiriwa na makosa mbalimbali.* Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




| | |
|---|---|
| i | Kutafsiri Sheria zilizotungwa na bunge. |
| ii | kutoa hukumu juu ya kesi mbali mbali |
| | zilizokwisha kusikilizwa |
| iii | Kusimamia ulipwaji wa fidia kwa watu walio- |
| | dhulumiwa mali zao |
| iv | Kusimamia, kulinda na kutetea haki |
| | za binadamu. |

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 1.

Aidha, watahiniwa 1,029 (22.0%) waliopata ufaulu wa wastani walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao. Wengi walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitoa majibu pungufu au maelezo dhaifu na hivyo kushindwa kupata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja mbali na kutoa majibu mawili sahihi alitaja pia majibu yasiyo sahihi kama; *kukata shauri* na *kutoa fidia;* hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwengine, watahiniwa 182 sawa na asilimia 3.9 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao (3.8%) waliopata kuanzia alama 0.5 hadi 1.5 walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana husika, hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine (0.1%) waliopata alama 0 hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu tofauti na kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliainisha matatizo mbalimbali yanayotokea katika jamii kwa hoja kama; *ufisadi*,

*ujambazi, kuachanisha ndoa* na *migogoro ya ardhi na mali*. Katika mfano mwingine, mtahiniwa aliandika; *kuwatetea, kuwalinda, kudai haki za wanafunzi* na *kulinda raia na mali zao*. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



1 i) Kutunga sheria.
ii) Kusimamia madaraka ya nchi
iii) Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi
iv) Kupanga bajeti.

**Kielelezo Na. 1.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa alijaribu kuainisha baadhi ya kazi za Bunge kwa hoja kama *kutunga sheria, kusimamia madaraka ya nchi* na *kupanga bajeti* pamoja na kazi za vyombo vya ulinzi na usalama katika nchi badala ya kazi za Mahakama Kuu ya Tanzania, hivyo alipata ufaulu hafifu.


### 2.1.2 Swali la 2: Dola

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa kifupi kazi nne za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama kiunganishi cha Serikali. Swali hili lilifanywa na watahiniwa wote 4,669 sawa na asilimia 100. Kati yao, watahiniwa 107 (2.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 701 (15.0%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 3,861 (82.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri, kwa kuwa asilimia 97.7 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Asilimia 82.7 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa juu katika swali hili waliweza kueleza kwa kifupi kazi tatu hadi nne za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya "Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar" kwa kuandika majibu sahihi. Majibu hayo yalikuwa kama ifuatavyo; *kutunga sheria, kusimamia serikali, kuwakilisha watu katika maamuzi ya kitaifa, kupitisha au kuidhinisha vyanzo vya mapato na matumizi ya serikali, kupitia na kuridhia mikataba ya kimataifa, kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, kumchagua Spika wa Bunge, kuchunguza mikataba na rushwa* na *kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali.* Kielelezo Na.2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


2

i/. Kutunga sheria. Sheria zote katika nchi kabla ya kutungwa hujadiliwa kwanza na kuidhinisha kwa Raisi aziwesaini ili ziwe kutumika.

ii Kuwakilisha watu. Bunge la tanzania huwakilisha watu kupitia wabunge waliochaguli wa katika majimbo.


iii Kupitisha na kuandaa bajeti ya nchi. bajeti za idara au wizara zote hupitishwa bungeni.

iv Kuidhinisha uteuzi wa waziri mkuu. Katika uteuzi wa waziri mkuu wabunge humpigia kura na kujua kama atakuwa amepita.

**Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 2.

Asilimia 15 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani, kati yao wapo waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine waliandika majibu pungufu kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alichanganya katika hoja zake kazi za Mahakama, kwa hoja kama; *kutafsiri sheria* na *kusimamia ulipwaji wa fidia*, hivyo alipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, kati yao asilimia 2.2 waliweza kutaja kazi moja tu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wengine waliweza kutaja aina mbili hadi tatu za kazi za Bunge bila maelezo. Aidha, asilimia 0.1 ya waliopata alama 0, kati yao walikuwepo ambao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu kazi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama: *kuongoza nchi, kuvunja kamati za bunge na kusaini mikataba mbalimbali*, majibu ambayo si sahihi kwa mujibu wa matakwa ya swali. Katika mfano mwingine, mtahiniwa aliandika; *kutafsiri sheria, kugawanya madaraka kwa kila mbunge* na *kumuapisha kiongozi wa nchi*. Kielelezo Na. 2.2. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.



| 2 | (a) Wabunge 232 wakuchaguliwa kwa kila jimbo |
|---|---|
| | (b) Wabunge wa viti maalum 152 wanawake |
| | (c) Mwanasheria Mkuu |
| | (d) Wabunge (5) tano wawakilishi kutoka Zanzibar. |
| | (e) Wabunge wakuteuliwa na Rais. |
| | |

**Kielelezo Na. 2.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa aliandika baadhi ya aina za wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala ya kufafanua kwa ufupi kazi nne za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo kupata alama 0.

### 2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu


Swali lilimtaka mtahiniwa kutofautisha kwa kutoa mifano kati ya jinsi na jinsia kwa kutumia hoja nne. Swali lilifanywa na watahiniwa 4, 669 sawa na asilimia 100. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa asilimia 61.8 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 13.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 25.0 walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa ni asilimia 38.2 ya watahiniwa pekee ndio waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4.


Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 2,885 (61.8%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5 katika swali hili. Baadhi yao asilimia 33.8 walishindwa kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa majibu pungufu na yenye udhaifu hivyo kupata kuanzia alama 0.5 hadi 1.5. Asilimia 28 waliopata alama 0 baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya jinsi na jinsia, hivyo kushindwa kutofautisha dhana hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama; *si rahisi kuyaona maumbile ya mwanamke kwa sababu husitiliwa, jinsi ni tabia ya mtu katika maisha yake kila siku.* Katika mfano mwingine, mtahiniwa alitofautisha dhana hizo kwa kuandika; *Jinsi ni vile mtu huishi katika maisha yake na jinsia ni maumbile aliyonayo mtu.* Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


3
i) Jinsia ni maumbile lakini jinsi ni hali ya mtu kutaka kufanya jambo kwa kufikiri
ii) Jinsia zipo za aina mbili (Kike na kiume) lakini
Jinsi huwa haina aina. (huwa si aina)
iii) Jinsia huwahusu viumbe lakini
Jinsi haihusiani na viumbe.
iv) Jinsia zinauwezo wa kuzaa au kunalisha lakini
Jinsi huwa hawezi kuzaa wala kunalisha.

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1 mtahiniwa alishindwa kutofautisha dhana ya jinsi na jinsi hivyo, alifafanua jinsia kama hali ya kimaumbile na jinsi kama hali ya kutenda jambo. Mtahiniwa alipata alama 0.

Aidha, asilimia 25 ya watahiniwa waliopata alama za juu katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Utamaduni Wetu*, hususan mada ndogo ya *masuala kuhusu maisha ya familia*. Watahiniwa hao waliweza kutoa majibu sahihi kwa kueleza tofauti ya jinsi na jinsia kwa kutumia vigezo vya maumbile na majukumu katika jamii husika. Kwa mfano baadhi yao waliandika *jinsi inahusiana na maumbile ya kibaolojia yaani ile hali ya kuwa mwanaume au mwanamke. Dhana ya mifano ya jinsi mwanamke/msichana anaweza kupata mimba, hedhi au kunyonyesha na tofauti hizi hazibadiliki. Kwa upande mwingine mwanaume/mvulana anaweza kusababisha mimba, hawezi kupata hedhi na hawezi kunyonyesha mtoto.* Jinsia inahusiana na *mahusiano na mgawanyo wa shughuli au majukumu kati ya wanaume/wavulana na wanawake/wasichana. Uhusiano wa kimajukumu unaundwa na jamii na hubadilika kulingana na jamii husika inavyobadilika. Kwa mfano katika jamii ya kimasai msichana anaweza kukamua maziwa ng'ombe wakati katika jamii nyingine hawezi.* Watahiniwa hao walidhihirisha kuelewa matakwa ya swali kama inavyoonekana kwenye sampuli ya jibu la mtahiniwa kwenye Kielelezo Na. 3.2.



| JINSI | JINSIA |
|---|---|
| (i) Utofauti wa kimaumbile yaani wasichana na wavulana | (i) utofauti wa mgawanyo wa majukumu katika shughuli za uzalishaji mali. |
| (ii) Huusisha viungo vya uzazi | (ii) Haihusishi viungo vya uzazi |
| (iii) Jinsia ya kike huzaa | (iii) Majukumu ya kulea watoto ni zaidi kwa wa akina mama. |
| (iv) Jinsi ya kiume huweza kutungisha mimba | (iv) Majukumu ya kutafuta chakula ni zaidi kwa baba. |


**Kielelezo Na. 3.2**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 3.

Kwa upande mwengine, watahiniwa 615 sawa na asilimia 13.2 waliopata alama za wastani katika swali hili walikuwa na mapungufu mbalimbali

katika majibu yao kama: uchanganyaji wa majibu sahihi na yasiyo sahihi, utoaji wa hoja pungufu ya nne zilizohitajika kwenye swali na kurudia majibu. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya wastani katika mada husika hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja pamoja na majibu sahihi alitoa pia majibu yasiyo sahihi kama: jinsi *inahusiana na maumbile pamoja na majukumu*, na *jinsia inahusika na mgawanyo wa kazi na viungo vya uzazi* bila maelezo yenye kutofautisha dhana zote mbili na hivyo alipata alama za wastani.

### 2.1.4 Swali la 4: Utamaduni Wetu


Swali hili lilikuwa na sehemu mbili, sehemu (a) ilimtaka mtahiniwa kumuelezea kiongozi mwadilifu katika muktadha wa somo la Uraia na sehemu (b) ilimtaka kuainisha mbinu tatu zinazoweza kutumika kurekebisha maadili mabaya katika jamii. Miongoni mwa watahiniwa 4,669 waliofanya swali hili, watahiniwa 524 (11.2%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa 981 (21.0%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 3,164 (67.8%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 88.8 walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Asilimia 67.8 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kumwelezea kiongozi mwadilifu kwa ufasaha katika sehemu (a) kwa majibu kama; ni *mfuasi wa tabia*, *mwenendo na matendo mema*

*yanayokubaliwa katika jamii fulani. Kiongozi mwadilifu anapaswa kuwa na sifa ya kuwa muwazi, mwenye maono, mwenye ujasiri, mwenye subira, mbunifu, mwajibikaji, mwenye kujituma, mwenye kuwasiliana vizuri na wenzake* na *mwenye nidhamu*. Aidha, katika sehemu (b) waliweza kuainisha mbinu zinazoweza kutumika kurekebisha maadili mabaya katika jamii. Mifano ya majibu sahihi iliyotolewa ni kama ifuatavyo: *kutoa elimu kwa jamii, kudhibiti na kusimamia vema maswala ya utandawazi, kutunga sheria na kanuni kwa ajili ya wale wote wanaoonekana kukiuka maadili mema, kuwepo na shughuli au kazi za uzalishaji mali, kudhibiti vijiwe na vilabu vya pombe pamoja na maeneo au majumba ya starehe, mitaala ya elimu kuanzia shule za awali mpaka elimu ya juu kuwe na umahiri unaohusiana na maaadili yanayokubaliwa na jamii husika* na *kuhusisha viongozi wa dini katika kukemea matendo yasiyofaa*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walielewa vema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



4 a) Kiongozi mwadilifu ni: Kiongozi anayefuata Kanuni na
Sheria na Kuelekeza Wajibu wake bila Kushurutishwa
Mfano Kuongoza na Kutatua changamoto.
(b) (i) Kutoa elimu juu ya madhara ya maadili mabaya
katika jamii mfano uvutaji wa sigara na matumizi ya madawa
ya kulevya kama pombe.
(ii) Kutunga kwa sheria na kanuni kali juu ya
Maadili mabaya katika jamii. Kwa kutoa adhabu kali mfa
kutozwa faini au kufungwa jera.
(iii) Kuhimiza mafundisho ya dini; Mazehebu huhi
biria watu injiri njema kila kuepuka vitendo vyote viovu
mfano uhoyo, ubakaji na wizi.

**Kielelezo Na. 4.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 4.

Aidha, asilimia 21 ya watahiniwa waliopata alama za wastani walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu dhana iliyoulizwa. Kati yao wapo waliojibu kwa usahihi upande mmoja wa swali na wengine walichanganya majibu sahihi

na yasiyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *kiongozi mwadilifu ni yule anayejiamini na nadhifu wakati wote;* ambalo lilikuwa jibu dhaifu. Mtahiniwa mwingine alichanganya mbinu zisizosahihi katika sehemu (b) kwa kuandika; *kuondoa ukoloni* na *kujiepusha na nchi za magharibi*; hivyo alipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, asilimia 11.2 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao (11%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa wengine (0.2%) waliopata alama 0, baadhi yao hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *kiongozi mwadilifu ni msimamizi au mpangaji wa malengo. Ni yule anayejali na kuthamini mawazo yake wakati wa vikao mbalimbali.* Sehemu (b) mtahiniwa aliandika majibu kama; *mahakama, vikao vya familia na jando* na *unyango*. Mtahiniwa mwingine katika sehemu hii aliandika hoja kama; *kutoa nafasi za uongozi*, *kupunguza watoto wa mitaani na kufukuzwa kazi,* hoja ambazo hazina uhusiano na majibu ya swali. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekwenda kinyume na matakwa ya swali.


(a) Ni kiongozi ambaye anajua malengo yote ya somola uraia


(b) (i) Nyimbo
(ii) Matembezi ya galari
(iii) Ziara

**Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alichanganya dhana ya kiongozi mwadilifu na mwalimu bora wa somo la Uraia. Vilvile katika sehemu (b) mtahiniwa aliandika mbinu mbalimbali za kufundishia somo la Uraia kwa ngazi mbalimbali badala ya kuainisha mbinu zinazoweza kutumika kurekebisha maadili mabaya katika jamii. Mtahiniwa alipata alama 0.

### 2.1.5 Swali la 5: Uchumi wa Tanzania


Swali lilimtaka mtahiniwa kuorodhesha vyanzo vinne vya mapato vinavyotegemewa katika Uchumi wa Taifa letu. Chati Na. 5 inaonesha muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa asilimia 0.6 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 6.3 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 93.1 walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 99.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 4,348 (93.1%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4 kwa kuwa waliweza kuorodhesha vyanzo vitatu hadi vinne vya mapato. Baadhi ya majibu sahihi yaliayoandikwa ni kama; *kodi, ushuru wa forodha, faini mbalimbali, kodi za leseni na paspoti, misaada mbalimbali, maliasili (utalii, madini, samaki nk), uwekezaji wa pamoja* na *biashara ya mazao.* Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Mambo yanayochangia kukua au kuporomoka kwa uchumi*. Vilevile walielewa vema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



5 Vyanzo vya mapato katika taifa letu;
i Kupitia kodi mbalimbali za wananchi za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja.
ii Tozo kutoka huduma mbalimbali za serikali za kijamii kupitia mashirika yake mfano TANESCO, huduma za maji.
iii Shughuli kuu za kiuchumi mfano utalii, Uchimbaji madini na hata usafirishaji mfano shirika la ndege la Tanzania (ATCL).
iv Mikopo na misaada mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**Kielelezo Na. 5.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 5.

Aidha, asilimia 6.3 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama; kutoa hoja pungufu na kuchaganya hoja sahihi na zisizo sahihi zilizosababisha wapate kuanzia alama2 hadi 2.5. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alichanganya hoja mbili zisizosahihi katika majibu yake kama; *hifadhi za mazingira* na *elimu*; bila ufafanuzi na hivyo kupata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa wachache (0.6%) walikuwa na ufaulu hafifu katika swali hili. Baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu vyanzo vinne vya mapato vinavyotegemewa katika uchumi wa Taifa letu, hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi hivyo walipata kuanzia alama 0.5 hadi 1.5. Watahiniwa wengine (0.1%) waliopata alama 0, baadhi yao hawakuwa na maarifa kuhusu dhana iliyoulizwa na wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *ruzuku kutoka serikalini, benki, mashirika mbalimbali* na *mamlaka ya mapato na matumizi (TRA).* Katika mfano mwingine, mtahiniwa aliandika hoja kama; *pato la taifa, pato la umma, pato la shirika na pato la nchi*, ambayo si majibu sahihi. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa

aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.



5 (i) Uchumi
Mfano kushirikiana katika masuala ya Uchumi nchi wanachama kwa kitoa vyakula, mifugo n.k
(ii) Utamaduni
Muingiliano wa Utamaduni na kukua kwa sayansi na teknolojia mfano Ulaji, Uvaaji n.k
(iii) Siasa
Nchi wanachama kutumia mfumo wa vyama vingi katika nchi zao na utawala wa kidemokrasia
(iv) Biashara
Kutegemeana katika kubadilishana bidhaa kwa mfano Tanzania kuwapa marekani maharage na marekani kuwapa Tanzania madawa ya hospitali

**Kielelezo Na. 5.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alieleza nyanja mbalimbali za maendeleo katika nchi badala ya kuorodhesha vyanzo vinne vya mapato vinavyotegemewa katika uchumi wa Taifa letu kwa hoja kama; kodi, ushuru wa forodha, faini mbalimbali, kodi za leseni na paspoti hivyo alipata alama 0.

### 2.1.6 Swali la 6: Uhusiano wa Kimataifa

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha misingi minne inayowezesha nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kutegemeana. Watahiniwa wote 4,669 (100%) walifanya swali hili. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 6.





**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 90.2 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 9.4 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 0.4 walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kuwa ni asilimia 9.8 pekee ya watahiniwa ndio walipata kuanzia alama 2 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 4,212 (90.2%) walipata ufaulu hafifu katika swali hili. Kati yao, asilimia 65.2 walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana nzima ya *Uhusiano wa Kimataifa* hususan katika mada ndogo ya *Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine*; na hivyo kuorodhesha hoja 1 au mbili zenye dosari zilizo sababisha kupata alama kuanzia 0.5 hadi 1.5. Wengine (25%) walipata alama 0 kwa kuwa baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa ya dhana husika, hivyo kutoa majibu yote yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *uchaguzi wa mara kwa mara, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kiuchumi* na *biashara.* Mtahiniwa mwengine aliandika; *maswala ya afya, maswala ya elimu, maswala ya ulinzi na usalama* na *maswala ya biashara*. Mtahiniwa huyu aliandika maeneo ya mahusiano kati ya Tanzania na nchi nyengine badala ya misingi inayowezesha nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kutegemeana. Katika mfano mwingine mtahiniwa aliandika; *kutoa mikopo kwa nchi nyingine, kukaribisha wawekezaji, kutoa misaada* na

*kuondoa vikwazo.* Kielelezo Na. 6 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


6
i/. Kuboresha miundombinu
ii/. Kuboresha na kukuza maendeleo ya sayansi na teknolojia
iii/. Kuweza kuboresha taaluma nchini
iv/. Kukuza na kudumisha ushirikiano kati ka nchi

**Kielelezo Na. 6**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali 6.

Katika Kielelezo Na. 6, mtahiniwa alielezea faida zinazoweza kupatikana kwa nchi kuwa mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kikanda na Umoja wa Mataifa badala ya kubainisha misingi minne kwa hoja kama; mataifa yote ni huru na sawa, mataifa yote ni lazima yaheshimu mikataba ya Umoja wa Mataifa, wanachama wote wanapaswa kusuluhisha tofauti zao kwa njia ya amani n.k. hivyo alipata alama 0.


Aidha, asilimia 9.4 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5, baadhi yao waliandika majibu pungufu ya manne yaliyohitajika kwenye swali na wengine walirudia jibu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja zisizo sahihi kwenye majibu yake kama; *usawa wa mataifa* na *uimarishaji wa maslahi ya nchi wanachama*, ambayo hayakuwa majibu sahihi. Mtahiniwa mwingine aliandika; *msingi wa utu* na *msingi wa kusaidiana*; hivyo alipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (0.4%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walikidhi matakwa ya swali kwa kubainisha misingi minne inayowezesha kutegemeana kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN). Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni kama; *mataifa yote ni huru na sawa, mataifa yote kuheshimu mikataba ya Umoja*

*wa Mataifa, wanachama wote kusuluhisha tofauti zao kwa njia ya Amani*. Na majibu mengine sahihi ni; *nchi wanachama kutopaswa kutishia au kutumia nguvu za kijeshi kwa nchi nyingine, Umoja wa Mtaifa kutopaswa kuingilia mambo ya ndani ya nchi wanachama isipokuwa kama kuna uvunjaji wa haki za binadamu* na *nchi wanachama kupaswa kuunga mkono shughuli zote za Umoja wa Mataifa.* Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya "Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine."

### 2.1.7 Swali la 7: Uhusiano wa Kimataifa

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha athari hasi nne za Tanzania kujiunga katika jumuiya za kimataifa. Swali lilifanywa na watahiniwa wote 4,669 (100%). Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*


Chati Na. 7 inaonesha kuwa, asilimia 15.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 55.3 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 28.8 walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 84.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 55.3 ya watahiniwa walipata ufaulu wa wastani (alama 2 hadi 2.5) kwa sababu walitoa hoja pungufu ya nne na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyosahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alichanganya hoja zisizo sahihi katika majibu yake kama; *mimba za utotoni* na *ongezeko la rushwa*, hivyo alipata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 28.8 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walikidhi matakwa ya swali kwa kubainisha athari hasi tatu hadi nne za Tanzania kujiunga katika jumuiya za kimataifa. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Maeneo ya Mahusiano ya Kimataifa*. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa ni kama; *Tanzania kubeba mzigo wa malipo ya ada za uanachama kwenye jumuiya ambazo Tanzania ni mwanachama, ukubwa wa gharama za uendeshaji wa ofisi zinazotumika na wawakilishi wetu katika jumuiya za kimataifa.* Majibu sahihi mengine ni*; kuondolewa au kupunguzwa kwa baadhi ya kodi za biashara, athari za kiusalama kutokana na mwingiliano wa watu kutoka mataifa wanachama na nchi kulazimika kutekeleza makubaliano ya wanachama hata kama haikubaliani kwa asilimia mia moja, tofauti ya sarafu, ngazi tofauti za kiuchumi na tofauti za kitamaduni na kiitikadi.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (15.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, ambapo baadhi yao walitaja mbinu pungufu ya mbili na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo kupata alama kuanzia alama 0.5 hadi 1.5. Katika kundi hili, walikuwepo waliorudia majibu, kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *gharama za kujenga ofisi za kibarozi, kuwalipa mishahara wafanyakazi katika nchi za kigeni, kuwasaidia watanzania wanaopatwa na shida katika nchi za kigeni bila* kujua kuwa majibu yote hayo yanaingia kwenye *gharama za uendeshaji wa ofisi zinazotumika na wa wakilishi wetu katika Jumuiya za kimataifa*. Watahiniwa wengine (4.4%) waliopata alama 0 walishindwa kutaja mbinu sahihi hata moja. Watahiniwa hao hawakuelewa vema matakwa ya swali ama hawakuwa na maarifa yoyote yanayohusiana na ushirikiano wa kimataifa. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika hoja zisizo sahihi kama; *kupungua kwa kasi ya maendeleo nchini, kupunguza nguvu kazi ya taifa* na *kushuka kwa thamani ya sarafu*.

Kielelezo Na. 7 ni sampuliya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.





**Kielelezo Na. 7**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7, mtahiniwa alitoa majibu yasioendana na matakwa ya swali. Mtahiniwa aliandika mambo ya kuzingatia kwa mtu kuwa raia au mtumishi mwadilifu badala ya kubainisha athari hasi nne za Tanzania kujiunga katika Jumuiya za kimataifa.

### 2.1.8 Swali la 8: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia/Kujifunzia Somo la Uraia


Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha sifa nne za machapisho bora ya ziada ya kufundishia somo la Uraia. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa asilimia 22.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 25.9 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 51.7 walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 77.6 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 2,414 (51.7%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kubainisha sifa tatu hadi nne za machapisho bora ya ziada ya kufundishia somo la Uraia. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu machapisho bora ya ziada hususan mada ndogo ya "Uchambuzi wa Machapisho ya Ziada". Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na watahiniwa ni kama; *yawe na uhusiano na mada inayofundishwa, yawe yameandikwa kwa lugha ya kiwango cha wanafunzi na yaendane na utamaduni wao.* Majibu mengine sahihi ni; *yawe yanapatikana katika mazingira yao, yasiwe na lugha ya upendeleo, matusi, au kupotosha ukweli wa jambo husika, yawe na maudhui yanayohamasisha wanafunzi kuwa wabunifu na kufikiri kwa kina* na *yawe na uelekeo wa kumfanya mwanafunzi apende kuchambua na kuyatafsiri.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



8 Sifa za machapisho bora ya uraia ya ziada ni;
i Yaendane na mada za kujifunza katika somo la uraia.
ii Yawe na maarifa, ujuzi na stadi za ziada ili mwanafunzi apate maarifa mpya zaidi.
iii Yawe yameandikwa kwa lugha rahisi ili kueleweka vizuri kwa wanafunzi mpangilio na mtiririko mzuri pia yasionyeshe ubaguzi kwa watumiaji
iv Yazingatie umri na uelewa wa wanafunzi walengwa husika.

**Kielelezo Na. 8.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 8.

Asilimia 25.9 ya watahiniwa walipata ufaulu wa wastani kwa sababu ya mapungufu mbalimbali katika majibu yao. Mapungufu hayo ni kama; kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kutoa hoja pungufu ya tatu na kurudia hoja. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alirudia hoja kwa kuandika; *yawe na uhusiano na mada inayofundishwa* na *yazingatie maudhui yanayofundishwa kwa wanafunzi*. Mtahiniwa alishindwa kuhusianisha dhana “mada” na “maudhui” katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji, hivyo alipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,045 (22.4%) waliopata ufaulu hafifu, kati yao asilimia 18.5 walikuwa na maarifa hafifu kuhusu machapisho bora ya ziada ya kufundishia somo la Uraia hivyo kutoa hoja pungufu ya tatu na wengine kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo kupata kuanzia alama 0.5 hadi 1.5. Watahiniwa wengine (3.9%) waliopata alama 0, baadhi yao hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika sifa za zana za kufundishia kwa hoja kama; *zinaonekana vizuri, zisiwe hatari kwa walengwa na ziwe na rangi za kuvutia*. Mtahiniwa mwingine aliandika mambo yanayopatikana katika kurasa ya umiliki wa kitabu kwa hoja kama; *mchapishaji wa chapisho hilo, mwandishi wa chapisho hilo, toleo la chapisho hilo na mwaka wa chapisho hilo*.

Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.



8
i/ Hutumika kama rejea
ii/ Hutumika kupata maarifa ya ziada
iii/ Hutumika kwa kujisomea
iv/ Hutumika kwa kujijengea tabia ya kusoma vitabu

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa alitaja faida za machapisho bora ya ziada ya kufundishia somo la Uraia badala ya sifa zake, hivyo alipata alama 0.

### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kuwa azimio la kazi linahusiana na andalio la somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia hoja nne. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 9.





**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa asilimia 1.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, asilimia 27.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 71.7 walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa asilimia 98.9.

Asilimia 71.7 ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kuthibitisha kuwa azimio la kazi linahusiana na andalio la somo katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walielewa vema matakwa ya swali. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa katika swali hili ni kama zifuatazo; *azimio la kazi ni chanzo cha andalio la somo, humwongoza mwalimu kupata zana za kufundishia/kujifunzia katika andalio la somo, humwongoza mwalimu katika kupata rejea, humsaidia mwalimu kupima mwendo kasi wa ufundishaji wa somo lake* na *pia*

*humwongoza mwalimu katika kupata mbinu na njia za kufudishia na kujifunzia.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi katika swali hili.


9 i/ Azimio la kazi linahusiana na andalio la somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwani mwalimu anapoandaa andalio la somo ni lazima awe na azimio la kazi.

ii/ Andalio la somo na azimio la kazi vinaonesha ni zana gani ambazo mwalimu anatakiwa atumie katika ufundishaji wake.

iii/ Azimio la kazi huonyesha zana za upimaji ambazo mwalimu anatakiwa kutumia kuwapima watoto baada ya kufundisha.


iv/ Azimio la kazi na andalio la somo vinahusiana katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwani kwa kupitia azimio la kazi mwalimu anaweza kujua atatumia muda gani katika ufundishaji wake wa muda fulani hivyo wakati anaandaa atajua atumie vipindi vingapi.

**Kielelezo Na. 9.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 9.

Asilimia 27.2 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walitaja hoja pungufu na wengine kurudia hoja zaidi ya mara moja. Aidha katika kundi hili wapo waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano mtahiniwa moja mbali na majibu sahihi aliyotoa aliandika majibu yasiyosahihi kama; *humfanya mwalimu kujiamini* na *humfanya mwalimu kutumia muda vizuri;* ambazo ni faida za andalio la kazi kwa mwalimu.

Kwa upande mwingine watahiniwa wachache (1.1%) waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao (0.9%) walitoa hoja pungufu ya mbili au walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na hivyo kupata kuanzia alama 0.5 hadi 1.5. Watahiniwa wengine (0.2%) walishindwa kabisa kuthibitisha kuwa azamio la kazi linahusiana na andalio la somo katika mchakato mzima wa ujifunzaji na ufundishaji. Watahinwa hao walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu dhana husika na hawakuelewa matakwa ya swali hivyo walipata alama 0. Kwa mfano mtahiniwa mmoja

aliandika; *vyote huandaliwa na mwalimu, vyote huonesha ujuzi, vyote hutumia umahiri mkuu.* Mtahiniwa alishindwa kuonesha uhusiano wa zana hizo katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika mfano mwingine mtahiniwa aliandika; *yanafanana katika muundo wake* na *yote ni faida kwa mwalimu*. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.



9
Uhusiano wa andalio la somo na Azimio la somo
i) Muhtasari
ii) Kiongozi cha mwalimu
iii) mwongozo wa mwalimu
iv) Rejea

**Kielelezo Na. 9.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa aliainisha maandiko mbalimbali muhimu ya kufundishia somo la Uraia badala ya kuthibitisha kuwa azimio la kazi linahusiana na andalio la somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.10 Swali la 10: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia mifano kueleza kwa ufupi aina nne za malighafi zinazotumika kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia kwa wanafunzi wa Darasa la Sita. Miongoni mwa watahiniwa 4,669 waliofanya swali hili, watahiniwa 1,441 (30.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 1,388 (29.7%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,840 (39.4%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa asilimia 69.1. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 39.4 ya watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4, walikuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya *Upatikanaji wa Zana*. Watahiniwa hao waliweza kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa hoja sahihi tatu hadi nne. Majibu sahihi ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *karatasi; mfano boksi/kasha, majani na udongo, katika kutengeneza zana za kubumba. Miti, katika kutengeneza zana za kuchonga. Udongo, katika kutengeneza zana za kufinyanga. Bango kitita, katika kutengeneza zana za kuchora* na *vitambaa, katika kutengeneza zana za kufumwa, kudarizi na kushonwa.* Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

| 10 | |
|---|---|
| | i/. Miti. Miti hutumika kutengeneza vifani |
| | vya vitu mbali mbali Mfano kifani |
| | cha raisi wa Tanzania Mwalimu |
| | julias kambarage nyerere |
| | ii/. Maboksi. Mwalimu anaweza kutum |
| | ia maboksi kuweza kuchora ramani |
| | ya Tanzania |
| | iii/. Vitambaa mbalimbali. hutumika kutengene |
| | za zana mbali'mbali mfano kifani cha |
| | nyoka |
| | iv/. Udongo mfinyanzi. huu hutumika kujenga |
| | makumbusho ya kihistoria |
| | |

**Kielelezo Na. 10.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 10.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 30.9 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu. Kati yao asilimia 24.3 walipata kuanzia alama 0.5 hadi 1.5, jambo linalodhihirisha hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya *Upatikanaji wa Zana,* hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya swali. Wengine (6.6%) baadhi yao hawakuwa na maarifa katika dhana husika na wengine kati yao hawakuelewa matakwa ya swali hivyo, kuandika majibu tofauti na mahitaji ya swali yaliyosababisha kupata alama 0. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *ramani, vitabu mbalimbali, kadi za familia* na *machungwa.* Mtahiniwa mwengine aliandika; *vitu halisi, mazao, chaki* na *penseli.* Watahiniwa hao walichanganya dhana ya zana na malighafi za kuundia zana. Katika mfano mwingine mtahiniwa aliandika; *muhtasari, andalio la somo, azimio la kazi na nukuu za somo;* ambayo ni maandiko muhimu katika maandalizi ya ufundishaji. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.

**10** i) Kuchora picha; mfano kama mwalimu ana fundisha mada ya familia ni lazima kuchora picha ya familia.
ii) Kutengeneza au kufaragua; mfano kama anafundisha katiba ya nchi lazima atafaragua zana hiyo.
iii) Kuunda; Mfano anafundisha mada ya utamaduni ataunda kitu kinachoonesha mambo ya utamaduni.
iv) Kukusanya; hivi ni vitu au zana ambazo Mwalimu anaweza kukusanya kutoka katika mazingira anayoishi.

**Kielelezo Na. 10.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alipata alama, 0 kwa kuwa aliandika mbinu mbalimbali za kupata zana za kufundishia na kujifunzia badala ya kueleza kwa kifupi aina nne za malighafi zinazotumika kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia.


Aidha, asilimia 29.7 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani. Ufaulu huo ni matokeo ya watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana iliyoulizwa, hivyo kuandika majibu pungufu, kuandika jibu bila kutoa mfano na wengine kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya majibu ambayo si sahihi kama; *vifani mbalimbali* na *vitu halisi*; hivyo alipata alama za wastani.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma na Utaalamu)

Katika sehemu hii, kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Aidha, mtahiniwa alifaulu kwa wastani endapo alipata kuanzia alama 6 hadi 10, na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

### 2.2.1 Swali la 11: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza mambo matano anayozingatia mwalimu wakati wa kufanya maandalizi ya andalio la somo na azimio la kazi la somo la Uraia. Chati Na.11 inaonesha muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.





**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa asilimia 15.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, asilimia 49.5 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 35.4 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa asilimia 84.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5.

Uchambuzi unaonesha kuwa, asilimia 49.5 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 6 hadi 10 katika swali hili, walikuwa na maarifa ya wastani katika dhana ya kuandaa andalio la somo na azimio la kazi. Baadhi yao walieleza hoja pungufu ya tano na wengine walitaja hoja sahihi bila maelezo. Aidha, wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano; mtahiniwa mmoja mbali na majibu sahihi, alichanganya majibu ambayo si sahihi kama; *daftari na kalamu* na *uchambuzi wa kitabu cha ziada*. Wengine walionesha kuwa na mapungufu mbalimbali katika insha zao kama kutoanza na utangulizi wala kuwa na hitimisho na miongoni mwao waliandika utangulizi na himitisho lisilo na uhusiano na swali na hivyo kupata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 35.4 ya watahiniwa walipata alama za juu katika swali hili. Watahiniwa hao walikidhi matakwa ya swali kwa kueleza mambo matano anayozingatia mwalimu wakati wa kufanya maandalizi ya andalio la somo na azimio la kazi. Baadhi ya hoja sahihi zilizoandikwa na watahiniwa hao ni kama; *walengwa husika, umri wa walengwa, uwezo wa kiakili, njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia, upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi hatua kwa hatua, zana sahihi za kufundishia na kujifunzia, kalenda ya shule, ratiba ya vipindi* na *muhtasari wa somo*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha katika mada husika na walielewa matakwa ya swali. Wengi kati yao walianza na utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Kwa upande mwingine, watahiniwa walifanya vizuri kutokana na kuwa dhana hii hufundishwa katika masomo yao mengine upande wa Utaalamu. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

| 11. | Azimio la kazi ni mpango kazi wa muda mrefu ambao mwalimu amejiwekea katika kufanikisha jambo fulani mfano Wiki, mwezi, muhula au mwaka hii huwezа kumsaidia mwalimu kufikia malengo ambayo amejiwekea. Andalio la somo: Ni mpango wa muda ambao amejiwekea mwalimu katika ufundishaji wake mfano katika kipindi kimoja au viwili au Wiki ili kuweza kufanikisha malengo ambayo amejiwekea. Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya maandalizi ya azimio la kazi na andalio la somo. Muhtasari wa somo husika: Muhtasari huweza kumsaidia mwalimu kufahamu idadi ya mada ambazo anatakiwa kuzifundisha katika ngazi fulani hivyo Muhtasari huweza kumfanya mwalimu kuandaa azimio ambalo huweza kumsaidia kufanya maandalizi ya somo. Kitabu cha kiada: Kitabu hiki huweza kumsaidia kuandaa au kuangalia mpangilio na mtiririko mzuri wa mada ambao anatakiwa kuufuata hivyo kitabu cha kiada huweza kumsaidia mwalimu kuona mpangilio na mtiririko mzuri wa mada ambao anatakiwa kuufuata katika kufundishia na kujifunzia. Kuzingatia kalenda ya shule: Kalenda hii huweza kumsaidia mwalimu kufahamu matukio mbalimbali ambayo huweza kufanyika katika shule hivyo katika kufanya maandalizi hayo huweza kumfanya mwalimu azimio lake kuweza kuendana vizuri na ratiba ya shule pamoja na matukio mbalimbali. |
|---|---|


11 Cont. Kuzingatia kalenda ya mwaka. Kalenda hii huwera kumfanya mwalimu kujua matukio au sherehe mbalimbali zinazofanyika katika vipindi mbalimbali vya mwaka mfano sikuku za kiserikali kama vile Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, sikukuu ya Wafanyakazi pamoja na sikukuu za kidini, mfano sikukuu ya Iddi, sikukuu ya pasaka hivyo huwera kumfanya mwalimu kuandaa andalio na azimio ambalo huendana na wakati pamoja na matukio mbalimbali.

Kuandaa mada kwa kuzingatia Umri wa walengwa: Hivyo mwalimu anapokuwa akiandaa andalio la somo pamoja na azimio hutakiwa kuzingatia Umri wa Walengwa hii huwera kumfanya awero kuandaa mada ambayo huendana na walengwa.


Uzingatiaji wa Upatikanaji wa zana mwalimu anapokuwa akiandaa andalio anatakiwa wa kuzingatia zana ambayo huwera kupatikana kwa urahisi pamoja na zana ambayo kila mwanafunzi anaielewa.

Kwa hiyo kwa mwalimu yoyote anapokuwa akiandaa andalio la somo pamoja na azimio la kazi anatakiwa kuthamini mambo sana, kuzingatia kalenda ya shule pamoja na kalenda ya mwaka ili kuweza kumfanya ufundishaji wake kuwa mzuri.

**Kielelezo Na. 11.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 11.

Aidha, asilimia 15.1 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana iliyoulizwa, hivyo baadhi yao walitoa majibu pungufu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, na hivyo kupata alama hafifu. Wengine (0.1%) waliopata alama 0, hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu kinyume na matakwa ya swali, kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika majibu kama; *kuandaa vifaa kama daftari na kalamu, anza na jina la shule, andika jina la mwalimu, andika jina la somo na Darasa* na *Chora Jedwali*. Mtahiniwa aliandika hatua za uandishi wa andalio la kazi badala ya kueleza mambo matano anayozingatia mwalimu wakati wa kufanya maandalizi ya andalio la somo na azimio la kazi la somo la Uraia. Kielelezo Na. 11.2 ni sehemu

ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali hili.


Andalio la somo; Ni taarifa anazoandaa mwalimu kabla ya kuingia kwenye kipindi kwa lengo la kumrahisishia shughuli nzima ya ufundishaji.

Azimio la kazi; Ni taarifa anazoandaa mwalimu za muda mrefu ili kumuongoza katika uandaaji wa andalio la somo. Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika uandaaji wa taarifa hizi;

Uandishi wa taarifa za awali; Mwalimu anapoandaa taarifa hizi hulakiwa kuzingatia uandishi wa taarifa zote za awali kama jina la shule, Jina la mwalimu, Somo, Darasa, Tarehe na muda ambao kipindi kinafundishwa


Uandishi wa taarifa za msingi; Aidha mwalimu hupaswa

**Kielelezo Na.11.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa alifafanua hatua za uandishi wa vipengele vya andalio la somo kwa hoja kama; uandishi wa taarifa za awali, uandishi wa taarifa za msingi, uandishi wa tafakuri, uandishi wa tathmini na uandishi wa maoni. Aidha, mtahiniwa aliandika utangulizi na hitimisho lililo sahihi na hivyo alipata alama 0.

### 2.2.2 Swali la 12: Utamaduni Wetu

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua misingi sita inayoweza kutumika kujenga familia za wanafunzi wenye ufaulu mzuri. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa asilimia 1.2 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, asilimia 16.4 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 82.4 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa asilimia 98.8.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi (82.4%) walipata ufaulu wa juu (alama 10.5 hadi 15). Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu misingi inayoweza kutumika kujenga familia zenye misingi bora ya maadili mema na walielewa matakwa ya swali na pia walitoa hoja sahihi kulingana na matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa katika swali hili ni kama; *uwepo wa amani katika familia, upendo, maadili mema, heshima, ushirikiano, uvumilivu* na *kuwa tayari kusameheana.* Kielelezo Na. 12.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

12 Maadili mema ni jumla ya mambo yote na tabia njema zinazo kubalika katika jamii. Mfano wa maadili mema ni kupekua watu mizigo, kuwa na heshima kusalimia na kufanya kazi kwa bidii. Na misingi bora ya maadili mema ni jumla ya mambo yote yanayofanywa na familia au jamii ambayo yanaifanya familia kuwa bora. Na ufaulu mzuri wa wanafunzi shuleni hutokana na maadili mema. Wanafunzi ambao wamefunzwa maadili mema na wazazi wao huwa na taaluma nzuri kuliko wale wasio na maadili mema. pia kunamisingi inayoweza kutumika kujenga familia za wanafunzi wenye ufaulu huo. Misingi hiyo ni kama ifuatayo:

Upendo na utu, upendo na utu ni msingi ya maadili mema ambayo huweza kutengeneza familia za wanafunzi wenye ufaulu huo. kwa sababu mtu katika familia akiwa na upendo na utu atakuwa anafanya mambo yanayo onesha upendo na utu kwa watu hao. Na baada ya kuonesha upendo kwa watu hao watakua wakimuombea mema na kumfanya mtu huyo awe na sifa nzuri na kupendwa na watu wengi. Mfano mtu anawapenda wenzie hawanyanyasi wala hawabagui katika masomo na katika familia basi mtu huyo atakuwa anajijengea uwezo mzuri wa kufaulu.

Uadilifu na kutii, uadilifu na kutii au utii husaidia sana katika ujenzi wa familia za wanafunzi wenye ufaulu mzuri. kwasababu mwanafunzi akiwa na uadilifu na utii atakuwa anafanya vizuri katika masomo yake kwani atakuwa anatii na kutimiza kwa wakati yale anayoambiwa afanye na wazazi wake na walimu wanao mfundisha shuleni. Mfano mwanafunzi anaambiwa awahi shule, akae darasani kwa utulivu, Asome kwa bidii na afanye mazoezi na mwanafunzi

**12 Cont.**

akayatendea kazi yote hayo yatamfanya mwanafunzi afanye vizuri na kufaulu.

Uvumilivu na kutokata tamaa, Uvumilivu pia ni miongoni mwa misingi ya maadili mema ambayo inaweza ikajenga familia ya watu au wanafunzi wanao faulu au wanaofanya vizuri. kwasababu mwanafunzi akiwa mvumilivu na mtu ambaye hakati tamaa basi atafanikiwa katika masomo yake. kwa mfano mwanafunzi anavumilia pale anapofanyiwa mambo ambayo hayapendezi na mwalimu au na mwanafunzi mwenzake kutokana na sababu fulani, na hakati tamaa pale anapo katishwa tamaa basi mwanafunzi huo atakuwa na maadili mema.

Heshima na kuheshimiana, Heshima ni muhimu sana na kuheshimiana ni muhimu sana. Heshima na kuheshimiana kunatakiwa kujitokeza katika jamii kwa watu wote bila kujali tofauti zao, na bila kujali huyu ni mkubwa na huyu ni mdogo. Heshima yenyewe hufuatwa na watu wote katika familia au jamii. Na watu wakiheshimiana huwa wanajenga familia ya wanafunzi wanao faulu vizuri. Kwasababu Mwanafunzi au mtu yeyote akiwa anaheshimu watu wote huwa anajitengenezea njia nzuri ya kufaulu mambo yake

Umoja na mshikamano, Umoja na mshikamano pia ni miongoni mwa misingi ya maadili mema ambayo yanaweza kujenga familia ya wanafunzi wanao fanya vizuri. Kwasababu watu au wanafunzi wakishikamana na wakawa na umoja katika kufanya mambo mbalimbali yakiwemo masuala ya elimu basi wanafunzi watakuwa wana uwezo mzuri wa kufanya vizuri katika masomo yao. Kwa mfano wanafunzi wanashirikiana katika kujisomea

**Kielelezo Na. 12.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 12.

Asilimia 16.4 ya watahiniwa waliopata alama za wastani katika swali hili, baadhi yao walishindwa kutoa maelezo sahihi katika kutetea baadhi ya hoja zao na wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye kujitosheleza. Miongoni mwao, wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na hivyo kupata alama pungufu na wengine walitoa hoja sahihi pasipo na ufafanuzi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *uwepo wa amani ya kutosha* bila maelezo ya kina kutetea hoja hiyo.

Kwa upande mwingine, asilimia 1.2 ya watahiniwa walishindwa swali hili na hivyo kupata alama 0 hadi 5.5. Baadhi ya watahiniwa hao (0.6%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo kutoa hoja dhaifu bila maelezo ya kina na wengine kati yao walitaja hoja bila kutoa ufafanuzi, utangulizi wala hitimisho hivyo kupata kuanzia alama 0.5 hadi 5.5. Wengine (0.6%) walibainika kukosa maarifa kabisa kuhusiana na dhana husika na hivyo kutoa majibu yasiyosahihi yaliyosababisha kushindwa kwao. Hata hivyo, watahiniwa wengine katika kundi hili hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu tofauti na dhana iliyoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *kuwapa motisha*, *utoaji wa elimu rika na kutokata tamaa*. Mtahiniwa mwingine aliandika; *kuoneana huruma, kujiepusha na makundi rika, afya bora* na *ugawaji wa kazi*. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

12

Misingi ya maadili mema; Ni aina ya misingi ambayo inafuata Sheria na kanuni zote zinazohitajika katika jamii inayotuzunguka. ifuatao ni misingi Sita iliyoweza kutumika kujenga familia ya wanafunzi wenye ufaulu mzuri ambayo ni pamoja na misingi ifuatayo.

Misingi ya ufundishaji na ujifunzaji inayozingatia ushirikishwaji wanafunzi katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji; msingi huu ni muhimu kutambua na mwalimu anapokuwa anafundisha iti kuweka hali sawa kwa pande mbili anazofundisha mfano jinsia ya kike na ya kiume.

Msingi wa ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia jinsia zote; Mwalimu anapokuwa anatumia msingi huu kwa ufundishaji wake huweza kuleta ari ya kujifunza kwa wanafunzi kutokana na wanafunzi kuwa na hali ya umoja katika kujifunza na sio kuwa na ubaguzi hivyo huweza kuwafanya wawe wanajiamini na kuweza kuwa na uwezo mkubwa wa kuwa na maarifa.

Msingi wa ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia kueleweka dhana ya umuhimu wa matumizi ya zana/nyenzo vya kufundishia na kujifunzia; hivyo kwa kupitia msingi huu mwalimu huweza kuwapa wanafunzi maarifa ya kutosha katika kujifunza na kuweza kuwajengea kumbukumbu endel

12 Cont.

elimu wanafunzi kuweza kuwa na ujuzi, stadi pamoja na maarifa ya kutosha.

Msingi wa ufundishaji na ujifunzaji unazingatia dhana rahisi kwenda katika dhana ngumu; pia huu ni msingi ambao mwalimu anapaswa kutumia wakati wa zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kuwajengea wanafunzi ari ya kutaka kujifunza na kuweza kuyafikia malengo mahususi aliyokuwa ameyakusudia.

Msingi wa ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia kukazia maarifa; mwalimu pia ni muhimu kutumia msingi huu wakati wa ufundishaji. Hii ni kwa sababu ya kuweza kuwaongezea maarifa na stadi katika ujifunzaji ili kusudi wanafunzi wasiweze kusahau na kuweza kuyafikia malengo makuu yaliyo kusudiwa.

Msingi unaozingatia uelewa wa utunzaji wa zana/vifaa na uhifadhi wa zana katika mazingira ya shuleni, nyumbani na katika jamii kwa ujumla; hii ni mojawapo ya ngazi bora ambayo mwalimu anapaswa kuitumia ili kuweza kuyafikia malengo makuu kwa sababu elimu anayokuwa anaipata mwanafunzi kupitia msingi huu humsaidia mwanafunzi anapokuwa nyumbani na hata pia katika jamii inayomzunguka.


Hitimisho; Ni vyema kwa walimu wote kuweza kutumia misingi hii katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji ili kuweza kuwapatia wana-

**Kielelezo Na.12.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 12.

Katika Kielelezo Na.12.2 mtahiniwa aliandika misingi ya ufundishaji wa somo la Uraia badala ya kufafanua misingi sita inayoweza kutumika kujenga familia za wanafunzi wenye ufaulu mzuri, hivyo alipata ufaulu hafifu.

### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji na Tathmini

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua ngazi sita za nyanja ya utambuzi kama zinavyotumika katika mchakato wa upimaji wa wanafunzi na kutoa mfano wa swali moja kwa kila ngazi. Kati ya watahiniwa 4,669 waliofanya swali hili, watahiniwa 1,133 (24.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa 1,036 (22.2%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 2,500 (53.5%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 75.7 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa Watahiniwa* katika Swali la 13

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 53.5 ya watahiniwa waliweza kutoa mfano wa swali moja kwa kila ngazi, kuchambua ngazi sita za nyanja ya utambuzi hivyo walipata ufaulu mzuri (alama 10.5 hadi 15). Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Zana za Upimaji katika somo la Uraia* na walielewa vema matakwa ya swali. Majibu sahihi katika swali hili ni kama ifuatavyo: *Ngazi ya Kukumbuka; Ngazi hii huhusisha kutambua au kutumia kumbukumbu. Mfano; Ainisha sababu kuu mbili za kukua kwa Uchumi nchini Tanzania, Ngazi ya Kufahamu; ngazi hii hutumika kuonesha kwa vitendo kuwa mwanafunzi anaelewa vya kutosha na alipanga kwa kufikiri zaidi. Mfano; Kwa ufupi eleza kwa nini Tanzania bado ni mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Toa hoja mbili* na

*Ngazi ya Kutumia; Hii ngazi huhusisha maswali yanayomtaka mwanafunzi kutumia habari anaiyoifahamu kupata jibu. Mfano; Kwa kutumia maarifa uliyopata katika dhana ya Alama za Taifa, unadhani wimbo wa Taifa huimbwa katika nyakati zipi? Elezea nyakati mbili*. Majibu mengine sahihi yalikuwa; *Ngazi ya Kuchambua; Hii ni ngazi inayomtaka mwanafunzi kufikiri kwa makini na kwa undani. Mfano; Unafikiri ni kwa nini kurithi wajane ni miongozi mwa mila potofu inayotakiwa kupigwa vita nchini Tanzania? Toa hoja mbili. Ngazi ya Kutathmini; Hii ni ngazi inayohusisha maswali yasiyo na jibu moja yanayohitaji kufikiri, kupima na kutathmini jibu. Mfano; Eleza faida nne za kutunza mazingira kwa maendeleo endelevu* na *Ngazi ya Kuunda; ngazi hii inahusu maswali kwa kujenga hoja kwa makini na sahihi zaidi. Mfano; Pangilia beti zifuatazo za Wimbo wa Taifa ili kupata mtiririko unaostahili.* Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

13


Nyanja ya Utambuzi ni mga kati ya nyanja tatu za upimaji ambayo inalenga kujua kama mwanafunzi anafahamu vitu gani katika ufundishwaji na ujifunzaji wake. Mara nyingi nyanja hii ya Utambuzi hutumika sana katika suala nzima la ufundishaji na ujifunzaji kwa Mwalimu na kwa mwanafunzi. Kwa sababu nyanja hii ndiyo hutumika kama kioo katika suala la upimaji kwa maeneo maalumu ya upimaji.

Zifuatazo ni ngazi za nyanja ya Utambuzi kama zinavyotumika katika upimaji.

Ngazi ya Maarifa, katika ngazi hii ya maarifa nyanja hii ya utambuzi imeweza kubaini kuwa ngazi hii itumike katika upimaji. Ngazi hii hulenga kujua maarifa aliyopata mwanafunzi mfano "Taja aina mbili za "Kasili". Je kama mwanafunzi anakumbuka maarifa hayo.

Ngazi ya ufahamu, ngazi hii tumika katika upimaji ili kupima mwanafunzi wake juu ya uelewa wa kitu fulani mfano: "Fupisha habari uliyosikia na kutaja wazo kuu katika habari hiyo", ambapo mwanafunzi hupimwa kama anaweza kuifahamu kufupisha habari hiyo.

Ngazi ya Matumizi, mwanafunzi hupimwa namna ambavyo anaweza kutumia maarifa aliyoyapata katika kujifunza na kama anaweza kuyatumia- mfano, "Eleza njia zilizo kupelekea kutokea kwa ugonjwa wa Ukimwi". Swali hili humpima mwanafunzi huyu kama anaweza akatumia maarifa aliyoyapata kujibu swali.


13 Cont.

Ngazi ya Uchambuzi Maswali katika ngazi hii humlenga mwanafunzi aweze kuchanganua kitu mbalimbali. Mfano wa Swali "Tofautisha kati seli ya mnyama na seli ya mmea". hapo mwanafunzi hupima ulinganifu na utofauti.

Ngazi ya tathmini, Mara nyingi ngazi hii huwa na pande mbili ambapo huja zinazo ndiyo au kubalika/kukataa Mfano wa Swali "Je, unafikiri kuna faida yoyote ya mwalimu kutumia zana katika ufundishaji?" Swali hilo humtaka mwanafunzi kuanza kufanya tathmini ya kutoa majibu.


Ngazi ya uundaji, Maswali yanayo ulizwa katika ngazi ya uundaji mara nyingi humpima mwanafunzi kama ana ubunifu katika gani katika ufundishaji mfano wa Swali "Fupisha habari uliyo soma kwa maneno yasiyozidi hamsini", humtaka mwalimu kutumia ngazi ya uundaji.

Hivyo ni vyema walimu watumie ngazi hizi za nyanja ya utambuzi katika kuunda maswali na kutunga maswali kwa kufuata mtiririko wake kamili, ili kuweza nyanja kama vile mwelekeo na stadi katika suala la upimaji.

**Kielelezo Na. 13.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 13.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 24.3 ya watahiniwa waliopata alama za chini katika swali hili, baadhi yao (18.2%) hawakuwa na maarifa ya kina kuhusu dhana iliyoulizwa na hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyosahihi.  Wengine (6.1%) baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kuandika majibu  yasiyohusiana na swali na wengine hawakuwa na

maarifa kabisa ya dhana iliyoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika zana za upimaji kwa hoja kama; *mazoezi, mitihani na majaribio.* Katika mfano mwingine mtahiniwa aliandika mambo ya kuzingatia katika mchakato wa upimaji wa mtoto kwa hoja kama; *umri wa mtoto, uwezo wa mtoto, utayari wa mtoto, maarifa ya awali ya mtoto n.k.* Watahiniwa hawa pia walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali, hivyo walipata alama hafifu. Kielelezo Na. 13.2 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechanganya maarifa na hivyo kushindwa swali hili.





**Kielelezo Na. 13.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 13.

Katika Kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alichambua aina za maswali zinazoweza kutumika kupima wanafunzi katika somo la Uraia badala ya kuchambua ngazi sita za Nyanja ya utambuzi kama zinavyotumika katika mchakato wa upimaji wa wanafunzi. Mtahiniwa alipata alama 0.

Aidha, asilimia 22.2 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani katika swali hili, baadhi yao waliweza kutoa utangulizi sahihi lakini walishindwa kuchambua vizuri hoja zao na wengine walitoa hoja pungufu na baadhi yao walitaja ngazi sahihi bila ufafanuzi. Katika kundi hili walikuwepo watahiniwa waliochambua ngazi bila mifano hivyo kukosa alama za mifano na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alichanganya majibu yasiyosahihi katika majibu yake kwa hoja kama; *utungaji* na *kueleza;* bila maelezo yenye kutia nguvu hoja hizo, hivyo alipata ufaulu wa wastani.

### 2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kuandaa hatua za somo kwa kuzingatia muundo wa andalio la somo la Uraia lenye kuhusisha vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji na upimaji wa mada ndogo ya "Sera na Mipango" kwa dakika 40. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili unaoneshwa katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa asilimia 22.6 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, asilimia 30.1 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 47.3 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa asilimia 77.4.

Uchambuzi unaonesha kuwa, asilimia 47.3 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 15 waliweza kuandaa muundo wa andalio la somo la Uraia kwa kuzingatia hatua za somo wenye kujumuisha vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji na upimaji. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha katika dhana ya *Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia* na walielewa vema matakwa ya swali. Mtiririko wa hatua sahihi ni kama ifuatavyo: *Utangulizi dakika 05, Ujuzi mpya dakika 20, Uimarishaji wa maarifa dakika 05, Tafakuri dakika 05, Hitimisho dakika 05* na *jumla dakika 40.* Kielelezo Na. 14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

| | Hatua | muda | V. vya ufundishaji | V. vya ujifunzaji | V. vya upimaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 40 | | | |
| | Utang | Dk 5 | -Kuanza kuwauli | - Wanafunzi - | - Kuuliza |
| | ulizi | | za wanafunzi | kujibu maswali | maswali. |
| | | | maswali ya kipindi | yaliyoulizwa | na kujibiwa |
| | | | kilichopita Ili- | na mwalimu | |
| | | | kuweza kuendele | | |
| | | | a na kipindi kingi | | |
| | | | ne. | | |
| | Kutamb | | . Kutafuta maari | . Wanafunzi | - mazoezi |
| | ulisha | Dk20 | fa waliyo nayo | kueleza ma- | - maswali |
| | maarifa | | wanafunzi kuhu | mbo wanayo | na majibu |
| | mapya | | su sera na mipa | yafahamu | - kuwadodo |
| | | | ngo ya uchumi. | kuhusu sera | sa wana- |
| | | | kwa kujadili | na mipango ya | funzi kuhu |
| | | | katika vikundi | uchumi wa taifa | su sera na |
| | | | | na kushirikisha maonzo | mipango ya uchu |

| 14 Cont. | Hatua | Muda | Vitendo vya ufundishaji | Vitendo vya ujifunzaji | Vitendo vya upimaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mwalimu- | Mwanafunzi- | - kuuliza |
| | Kuimari | Dk 5 | kuwawezesha | kusikiliza- | maswali |
| | Sha maarifa | | wanafunzi | na kuchukua | - zoezi |
| | mapya | | kujua maana | nukuu juu | |
| | | | ya Sera na | ya maarifa | |
| | | | mipango ya | mapya anayo | |
| | | | uchumi na | yatoa kwa | |
| | | | umuhimu- | wanafunzi | |
| | | | wake kwa | | |
| | | | kutaria ma | | |
| | | | arifa | | |
| | | | | | -kuuliza |
| | | | Mwalimu- | Mwanafunzi | - maswali |
| | Tafakuri | Dk 5 | kufanya- | kuweza kuji | |
| | | | tafakuri ya | bu maswali- | - kueleza- |
| | | | Somo lake- | yaliyoulizwa | maana na |
| | | | kwa kuuliza | kuhusu mada- | umuhimu |
| | | | maswali | waliyosoma | wa sera ya |
| | | | | | mpango wa |
| | | | | | uchumi. |
| | | | Kuhitimisha | kujibu maswa | |
| | Hitimisho | Dk 5 | Somo kwa | ali ya mwali | - mazoezi |
| | | | kuuliza sehem | kwa usahihi | - majaribio |
| | | | u ambayo hai | na kuuliza- | |
| | | | jaeleweka | maswali kwa mwalimu | |


**Kielelezo Na. 14.1**: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa aliweza kuandaa muundo wa andalio la somo la Uraia alijumuisha vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji na upimaji kwa kuzingatia hatua za somo. Pia mtahiniwa aliweza kugawa muda kwa usahihi kulingana na shughuli hivyo alipata ufaulu mzuri.

Aidha, badhi ya asilimia 30.1 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani katika swali hili, waliweza kuainisha hatua na muda kwa usahhi lakini walishindwa kubainisha vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji na upimaji

kulingana na mada na hatua husika. Wengine walifafanua hatua pungufu na wengi kati yao waliacha hatua ya *tafakur*i. Walikuwepo waliochanganya utangulizi kuwa hatua ya pili na ujuzi mpya kuanza.

Kwa upande mwingine, baadhi ya asilimia 22.6 ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu, (8%) hawakuwa na maarifa ya kina kuhusu dhana iliyoulizwa na hivyo walichambua hatua pungufu zilizosababisha kupata alama kuanzia 0.5 hadi 5.5. Halikadhalika, watahiniwa wengine (14.6%) hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kuandika majibu yasiyohusiana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mambo ya kuzingatia katika kutengeneza andalio la somo kwa hoja kama; *maudhui ya somo*, *njia na mbinu za ufundishaji*, *muda wa ufundishaji* na *maoni*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama; *kuakisi*, *shughuli za kutendwa na mwalimu*, *shughuli za kutendwa na mwanafunzi*, *tathmini ya kujifunza*, *viashiria pendekezwa*, *maoni ya ufundishaji* na *matumizi ya zana na njia na mbinu za ufundishaji*. Kwa kuzingatia muundo wa andalio la somo hizo zote sio hatua za somo zinazopaswa kuzingatiwa. Aidha, watahiniwa wengi katika kundi hili walishindwa kufuata taratibu za uandishi wa andalio la somo kwa kuhusisha mgawanyo wa muda, mfululizo sahihi wa hatua pamoja na mgawanyo wa mada ndogo iliyotolewa kama mwongozo. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


14

Andalio la somo ni mpango kazi anao
Andaa mwalimu kwa kufundishi kwa kipendi
cha muda mfupi ili kukamilisha swalo la
Ufundishaji. Zifuatazo ni hatua za somo kwa
kuzingatia vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji
Kutafuta au kuandika andalio la
Somo; hili ni muhimu sana hasa katika ufundishaji
na ujifunzaji na ni hatua moja wapo ya somo

Kuandaa nukuu za somo; hayo ni
Mambo muhimu yanayomuwezesha mwalimu kufundi
sha na pia kufikia malengo aliyokusudia na
pia ni hatua ya somo

Kuandaa mbinu za kufundishia; Mbinu
ziandaliwe kulingana na mada inayosema sera
na mipango ya uchumi mbinu pia iendane
na uelewa wa wanafunzi

Kuandaa zana za kufundishia;
Zana pia ziendane na uelewa wa wanafunzi pia
ziendane na mada husika kwan inasaidia
Kurahisisha ufundishaji wa somo

Kwahiyo; Hatua za ufundishaji wa
Somo zifuatwe ili kuboresha ufundishaji na
Ujifunzaji na kufanya tathmini ya Somo

**Kielelezo Na. 14.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alifafanua maandalizi ya jumla anayotakiwa kufaya mwalimu kabla ya kufundisha darasani badala ya kuandaa muundo wa andalio la somo la Uraia kwa kuzingatia hatua za

somo wenye kujumuisha vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji na upimaji. Mtahiniwa hakuwa na maarifa ya dhana iliyoulizwa hivyo aliapata alama 0.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Uraia ulitahini mada nane (8). Uchambuzi wa takwimu za matokeo unaonesha kuwa, mada sita (6) kati ya nane (8) zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada hizo ni: Uchumi wa Tanzania (99.40%), Dola (96.90%), Maandalizi ya Kufundishia Somo la Uraia (87.06%), Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia (77.60%), Upimaji na Tathmini (75.70%) na Utamaduni Wetu (75.26%). Ufaulu huu umesababishwa na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada zilizoulizwa na uwezo wa kutafsiri kwa usahihi matakwa ya swali.

Hata hivyo, mada za Zana za Kufundishia na Kujifunzia na Uhusiano wa Kimataifa zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu wa asilimia 69.10 na 46.95 mtawalia. Ufaulu huo wa wastani ulisababishwa na watahiniwa wengi kutokuwa na umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki hususan katika mada ndogo ya "Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine" na "Masuala kuhusu maisha ya familia." Muhtasari wa ufaulu wa mada umeoneshwa katika Kiambatanisho A.

Uchambuzi zaidi ulifanyika kwa kuangalia ulinganifu wa kiwango cha ufaulu wa mada kati ya mwaka 2021 na 2022. Ilibainika kuwa, kiwango cha ufaulu katika mada ya Dola na Uchumi wa Tanzania kiliongezeka kwa asilimia 30.3 na 3.5 mtawalia. Aidha, uchambuzi wa mada za Uhusiano wa Kimataifa, Zana za Kufundishia na Kujifunzia, Upimaji na Tathmini, Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia, Utamaduni Wetu na Maandalizi ya kufundishia somo la Uraia kilishuka kwa asilimia 41.7, 23.7, 22.1, 21.4, 15.2 na 7.71 mtawalia. Ulinganifu wa ufaulu wa mada kati ya mwaka 2021 na 2022 umeoneshwa katika Kiambatisho B.

## 4.0 HITIMISHO

Ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa 612 Uraia 2022 ni mzuri kwa kuwa, asilimia 99.81 ya watahiniwa waliofanya Mtihani walipata wastani wa alama 40 na Zaidi. Aidha ufaulu umepungua kwa asilimia 0.14 ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2021 ambapo asilimia 99.95 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuongeza kiwango cha kufaulu katika mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani hususan kipengele cha *Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine* na *Masuala kuhusu maisha ya familia* inashauriwa kuwa:

(a) Walimu wanafunzi wahimizwe kujisomea makala na machapisho mbalimbali yanayohusu dhana ya Misingi inayoongoza uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine na Masuala kuhusu maisha ya familia ili kuwajengea umahiri na maarifa ya kina katika dhana hiyo.

(b) Ufundishaji na ujifunzaji katika mada hizi utumie mbinu shirikishi ili kuwajengea walimu tarajali uwezo wa kujibu maswali kulingana na matakwa ya swali hususan; Majadiliano katika vikundi na mawasilisho, Mdahalo, kisa mafunzo, igizo dhima na mapitio ya machapisho kupitia tovuti mbalimbali na kanda za video.

(c) Wakufunzi wajenge tabia ya kutoa mazoezi, majaribio na mitihani ya mara kwa mara ikiwa ya ujirani mwema au kikanda ili walimu wanafunzi wapate uzoefu wa namna za kuulizwa na kujibu maswali yenye kupima umahiri.

*Kiambatisho A*

**MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA URAIA**

| Na. | Mada | Na. ya swali | Ufaulu katika kila Swali (%) | Wastani wa ufaulu katika kila mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Uchumi wa Tanzania | 5 | 99.4 | 99.40 | Vizuri |
| 2. | Dola | 1 | 96.1 | 96.90 | Vizuri |
| | | 2 | 97.7 | | |
| 3. | Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia | 9 | 98.9 | 87.06 | Vizuri |
| | | 11 | 84.9 | | |
| | | 14 | 77.4 | | |
| 4. | Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia | 8 | 77.6 | 77.60 | Vizuri |
| 5. | Upimaji na Tathmini | 13 | 75.7 | 75.70 | Vizuri |
| 6. | Utamaduni Wetu | 3 | 38.2 | 75.26 | Vizuri |
| | | 4 | 88.8 | | |
| | | 12 | 98.8 | | |
| 7. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 10 | 69.1 | 69.10 | Wastani |
| 8. | Uhusiano wa Kimataifa | 6 | 9.8 | 46.95 | Wastani |
| | | 7 | 84.1 | | |

*Kiambatisho B*

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2021 NA 2022

